**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)**


**MKOA WA RUVUMA**
**NAMBA ZA SIMU**
**Ofisini:** **0621981409**
**Mkuu wa shule:** **0753412885/0621981409**
**Makamu mkuu wa shule:** **0753708767/0659679828**

**SHULE YA SEKONDARI MATAKA,**
**S.L.P 175,**
**TUNDURU**
**TAREHE......................................**

**Kumb. Na. MDSS/UKV/99/VOL/2022**
**E-mail: matakasecondary@gmail.com**


**Mzazi/mlezi wa mwanafunzi**
**.....................................................**
**.....................................................**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA TANO MWAKA 2022 KATIKA SHULE YA SEKONDARI MATAKA,HALMASHAURI YA WILAYA YA TUNDURU,MKOA WA RUVUMA**

Sawa na mada tajwa hapo juu.
Ninayo furaha kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule tajwa hapo juu kuanzia july 2022 kwa mchepuo wa ..........................

Shule ya sekondari mataka ni ya kutwa kwa wanafunzi wa kidato cha kwanza hadi cha nne na bweni kwa kidato cha tano na sita. Pia shule ni mchanganyiko kwa kidato cha kwanza hadi cha nne na wavulana pekee kwa kidato cha tano na sita.

Shule inapatikana Tunduru **mjini kilometa tatu (03)** kutoka stand kuu ya mabasi. Unapokuja shuleni ukitokea stand kuu unatakiwa kuelekea barabara iendayo masasi, baada ya **kuvuka daraja la mto mlingoti** upande wa kushoto kwa kuelekea masasi utaona kibao cha shule ya sekondari mataka kikielekeza mahali shule ilipo. Ni **umbali wa mita 700** kutoka barabara kuu iendayo masasi.
Muhula wa masomo unatarajia kuanza ........................... hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe..............................na mwisho wa kuripoti shule ni tarehe..............................

Wanajumuiya ya mataka sekondari wanakupongeza sana na kukukaribisha hapa shuleni kwa lengo la kujifunza yaliyo mema kwa manufaa ya taifa letu la Tanzania. **"kumbuka elimu ndiyo mkombozi wako, mshike usimuache aende bila wewe kupata faida kutoka kwake"**

Pamoja na barua hii, nimeambatanisha na fomu , **fomu na. 1 inahusu kujiunga na shule, fomu na. 2 inahusu kukubali au kukataa kujiunga na shule, fomu na. 3 medical form** na sheria za shule.
Karibu sana.

**"YATUPASA TUBADILIKE"**

**.......................................**

**MKUU WA SHULE**

HEADMASTER
MATAKA SECONDARY
P.O.BOX 175
TUNDURU

**MAAGIZO MUHIMU YA SHULE**

Maagizo yafuatayo ni muhimu kuyakamilisha ikiwa ni sehemu maandalizi ya kujiunga na kidato cha tano kwa mwaka 2022

1. Sare za shule
    - Shati nyeupe mikono mirefu pair 2 (tetron) zenye kola shingoni na siyo za kubana, kizibao rangi ya ugolo.
    - Suruali 2 na tai 2 za rangi ya ugolo ( **MUHIMU KUZINGATIA** Suruali zote zinashonwa shuleni kwa gharama ya shilingi 50,000/=) ,malipo yatapokelewa wakati wa usajili kwenye ofisi ya makamu mkuu wa shule.
    - T-SHIRT 01(zinapatikana shuleni kwa gharama ya sh 15,000/=) malipo yatafanyika wakati wa kusajiliwa kwenye ofisi ya makamu mkuu wa shule
    - Mkanda mweusi jozi 2
    - Viatu vya kamba rangi nyeusi jozi mbili na soksi nyeupe jozi 2
    - Sweta rangi ya ugolo
    - Nguo za michezo na mazoezi ambazo ni bukta na tshirt za blue jozi 2, viatu vya michezo (raba), tracksuit rangi ya blue.
    - Nguo za kazi ambazo ni suruali 2 na tshirt 2 za blue zisizo na maandishi.

**MUHIMU KUZINGATIA:** ***Nguo za nyumbani haziruhusiwi shuleni.***

***Simu za mkononi haziruhusiwi shuleni, mwanafunzi akikutwa na simu hataendelea na masomo.***

**2. Michango ya shule:**

- Ada ya shule Tsh 70,000 kwa mwaka, 35,000/- kwa muhula.
- Taaluma Tsh 20,000 kwa mwaka , 10,000 kwa muhula.
- Malipo ya wapishi, walinzi na vibarua wengine Tsh 30,000/= kwa mwaka, 15,000/- kwa muhula
- Afya Tsh 10,000 ikiwa Tsh 5000/= huduma ya kwanza na Tshs 5000/= Bima ya Afya. Kama mwanafunzi ana Bima ya Afya anapaswa kulipa Tshs 5000/= pekee ya huduma ya kwanza.
- Ukarabati wa samani Tsh 15,000/=
- Tahadhali Tsh 5000/= (haitarudishwa)
- Kitambulisho na picha Tsh 6000/=
- Mtihani wa Mock kidato cha Sita Tshs 20,000/=
- Welcome form five Tsh 5000
- Mahafari kidato cha sita 5000

**NB. Malipo yote ya ada na michango mingine yafanyike kupitia akaunti ya bank namba 70901100053 bank ya NMB jina la akaunti MATAKA SEKONDARI. Risiti za bank (BPS) ziwasilishwe ofisi ya mhasibu wa shule pindi unaripoti shule**

3. vifaa na maagizo mengine

- Godoro la ft 2.5, mto na foronya rangi ya bluu.
- Shuka mbili rangi ya bluu, chandarua na blanket 1
- Sanduku imara lenye kufuli kwa matumizi ya kuhifadhia vifaa vyake muhimu
- Kwa mchepuo wa HGK anapaswa kuja na vifaa vifuatavyo:-

  Jembe 1 lenye mpini, reki na fagio ngumu.
- Kwa mchepuo wa HKL anapaswa kuja na vifaa vifuatavyo:-

  Jembe 1 lenye mpini,fyekeo, fagio laini na drayer ya kudekia.(kusukumia maji)
- Kwa mchepuo wa HGL anapaswa kuja na vifaa vifuatavyo:-

  Jembe 1 lenye mpini, shoka lenye mpini na panga.
- Ndoo 2 za lita 10, kandambili na taulo
- Dawa ya kusafisha choo lita 5 kwa mwaka
- Vyombo vya chakula kama sahani kikombe na kijiko (visivyo vya plastic)
- Nakala ya cheti cha kuzaliwa, kuhitimu kidato cha nne ( leaving certificate) na hati ya matokeo ya kidato cha nne (result slip)
- Ream A4 02 kwa mwaka
- Daftari 12 kubwa (counter book)
- Picha ya hivi karibuni ya mwanafunzi na wazazi/walezi wake
- Fedha za kumtosheleza kwa matumizi ya kawaida ya mwanafunzi kama vile kununua kalamu, kutoa nakala ya matini mbalimbali, mafuta ya kupaka, sabuni n.k
- Kumbuka kununua vitabu vya ziada kwa matumizi yake binafsi
- Kumbuka kujaza fomu zote ambazo umetumiwa kasha kabidhi fomu zote ofisi ya msajili wa **shule (makamu mkuu wa shule)**

## 4. SHERIA ZA SHULE

Shule ni mahali ambapo kijana hujipatia elimu na mategemeo ya kujitayarisha kwa maisha yake ya baadae. Hivyo kwa kutambua umuhimu wa shule, kijana anatakiwa kutumia uwezo wake wote kujiendeleza kielimu na maarifa ya kukabiliana na Mazingira yanayomzunguka. Anapaswa kuzingatia Nidhamu, utii na kuishi vizuri katika jumiya ya shule na nje ya shule.

Ili kuhakikisha lengo la hilo linafikiwa, SHERIA ZA SHULE zimewekwa, sheria ambazo ni muhimu kwani zina jukumu la kulinda haki na utu wa kila mwanafunzi na sifa nzuri ya shule. ikumbukwe pia walimu na wafanyakazi wasio walimu ni Viongozi na walezi wa Wanafunzi wote shuleni. Hivyo kila mmoja anawajibu wa kuhakikisha maisha ya kila mwanafunzi yanakuwa mazuri shuleni na maisha baada ya shule.

Kwa vyovyote vile, nia ya shule kama taasisi ni kujenga busara. Nidhamu na uzalendo wa mwanafunzi kwa nyakati za sasa na baadae endapo atakua raia mwema au endapo atashika madaraka yeyote. Pia inamuandaa kijana kuwa ni raia mwenye kutii sheria na kutovunja ahadi. ushirikiano na hisani. licha ya kumuendeleza kitaaluma darasani. Kwa kuzingatia hayo, shule itamlea kila mwanafunzi na kumkukuza katika misingi ya jamii katika hali yake ya Uhuru. utu. usawa na kuthamini wengine katika jamii ndani na nje ya shule.

Kwa mafunzo yenye miongozo. yatamfanya mwanafunzi amthamini mtu yeyote kwa siku zijazo siyo kwa sababu ya elimu yake tu, bali hata kwa matendo yake mazuri na imani yake.

Kwa lengo la kumpatia mwanafunzi misingi hiyo inayofaa katika maisha yake ya baadae. anapaswa kuzingatia **sheria za shule** zifuatazo:

1) Kila mwanafunzi anapaswa kutumia akili zake za asili na busara katika kufanya uamuzi wa vitendo mbalimbali awapo shuleni na nje ya shule.

2) Kuwahi mahala popote anapohitajika.
    - Kila mwanafunzi anapaswa kuamka asubuhi mapema kwa kufanya mazoezi (mchaka mchaka) kisha kufanya Usafi wa Mazingira na Usafi binafsi na kuwahi paredi saa 1.30 asubuhi. Kuchelewa kutekeleza haya ni kosa.
    - Kutii kengere ya paredi na maeneo mengine kila anapohitajika.
    - Mwanafunzi anapaswa kuwahi (kukimbia) kila anapoitwa na mwalimu au kiongozi wa Wanafunzi.

3) Kuwa na heshima.
   Mwanafunzi anapaswa kumheshimu mtu yeyote bila kujali umri, wadhifa na uwezo wa aina yeyote. Hivyo ni lazima kwa mwanafunzi kusalimia kwa watu wote kwa kuzingatia umri wao.

4) Lazima kuvaa sare za shule
   Ni kosa kubwa kwa mwanafunzi kutovaa sare za shule awapo shule, pia nje ya shule akiwa na ruhusa maalum. Ni marufuku kuvaa kofia, ndala na kuwa na mapambo ya aina yoyote kama vile mkufu, bangili, pete nk.

5) Utoro.
   Ni kosa kubwa kwa mwanafunzi kutoroka shuleni/ darasani. Mwanafunzi anapaswa kuwa darasani/ shuleni kwa wakati wote. Hivyo mwanafunzi haruhusiwi kutoka nje ya mipaka ya shule bila ruhusa/ kibali toka kwa mwalimu wa zamu.

6) Utunzaji wa vifaa vya shule

Ni kosa kwa mwanafunzi kuharibu mali yake na mali ya shule kama vile vitabu, viti, madawati n.k.

7) Wizi

Ni kosa kwa mwanafunzi kuiba au kushiriki katika kitendo cha wizi wa aina yeyote.

8) Utulivu na amani

- Ni kosa kwa mwanafunzi kupiga **KELELE** akiwa darasaniau hata nje ya darasa katika Mazingira ya shule.
- Ni koswa kwa mwanafunzi kupiga au kupigana au kuleta uchochezi wa aina yeyote.
- Ni kosa kwa mwanafunzi kufanya uasherati.

9) Bidii katika Kazi

Kufanya kazi ni wajibu kwa kila mwanafunzi, hivyo ni kosa kwa mwanafunzi kutofanya au kutegea kazi za mikono ambazo zitakuwa zinapangwa na Viongozi kila siku.

10) Taaluma

Ni kosa kwa mwanafunzi kutofanya kazi za darasani ambazo zimetolewa na walimu/ Viongozi pia kutohudhria darasani bila sababu za msingi.

11) Ulevi na Uvutaji Sigara

- Ni kosa kubwa kwa mwanafunzi kuvuta, kuuza sigara au bangi au kutumia kilevi cha aina yeyote.
- Ni kosa kwa mwanafunzi kuonekana maeneo ya starehe, kama vile bar, disco, nyumba za wageni.

12) Ni kosa kwa mwanafunzi kuonekana kwenye nyumba za walimu au wafanyakazi wasio walimu bila ruhusa.

13) 13) ni marufuku kwa mwanafunzi kufanya vitendo viovu vinavyo weza kudhalilisha na kushusha heshima au kusababisha sifa mbaya kwa shule.

**MAKOSA YATAKAYO SABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.**

i) Wizi

ii) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/ utoro

iii) Kugoma au kuhamasisha mgomo

iv) Kutoa lugha chafu kwa Wanafunzi wenzake, walimu/ walezi na jamii kwa ujumla.

v) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote Yule.

vi) Kusuka nywele au kunyoa nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.

vii) Kufuga ndevu

viii) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.

ix) Uvutaji sigara.

x) Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoa au kuolewa.

xi) Kupata ujauzito au kutoa mimba

xii) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.

xiii) Kusababisha mimba.

xiv) Kutembelea nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni.

xv) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika Mazingira ya shule.

xvi) Kudharau bendera ya taifa.

xvii) Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k

xviii) Uharaibifu wa mali ya Umma kwa makusudi.

**5. Viambatanisho na Fomu Muhimu**

a) Fomu ya uchunguzi wa Afya ya Mwanafunzi ( Medical Examination Form). Ijazwe na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali.

b) Fomu ya kukubali ( Mkataba) wa kujiunga na shule na mkataba wa kutoshiriki mgomo, fujo na makosa ya jinai. Iwe imesainiwa na kukubariwa na Mzazi/mlezi.

c) Fomu yenye taarifa muihimu za mwanafunzi na mzazi au walezi ambao wataruhusiwa kumtembelea mwanafunzi awapo shuleni. Ni vema kuambatanisha picha za ndugu ambao watatambulishwa shuleni.

**KARIBU SANA MATAKA SEKONDARI**

.....................................

**NIVER R. MBUNDA,**

**MKUU WA SHULE.**

HEADMASTER
SECONDARY
P.O.BOX 175

**SHULE YA SEKONDARI MATAKA**
**S.L.P 175 TUNDURU.**
**FOMU YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MATAKA**
**TAARAFA ZA MWANAFUNZI**

Jina kamili la mwanafunzi:

Taifa.................................Mkoa.................................Wilaya........................

Tarehe ya kuzaliwa.........................................

Lugha unayozungumza nyumbani.........................................Kabila................................

Jina kamili la baba.................................................Amefariki /Hai(kata isiyo husika)

Jina kamili la mama...............................................Amefariki/hai(kata isiyohusika)

Jina kamili la mlezi(kama huna wazazi)...........................................................

Uhusiano na Mlezi..............................................................

Kazi ya Baba..........................................kazi ya Mama...............................kazi ya Mlezi..............................

Je umewahikuwa kiongozi shule uliyotoka?NDIYO/HAPANA.Kama ndiyo kiongozi wa Njanja ipi?...............................

Michezo uipendayo:1......................................... 2.........................................
3.........................................Unamatatizo yoyote ya kiafya?NDIYO/HAPANA.Kama ndiyo taja

...........................................................................................................................................

...........................................................................................................................................

Mawasiliano ya sasa ya mzazi au mlezi wako:

Jina...................................................................

Sanduku la barua.............................................

Namba ya simu................................................

| | | |
|---|---|---|
| ................................................ | ................................................ | ................................................ |
| **Jina la mwanafunzi** | **Saini** | **Tarehe** |

FOMU KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MATAKA.

A)Mwanafunzi.

Nimesoma na kuzielewa sheria na taratibu zote za shule na ninakubali/sikubaliani (kata isiyohusika) kusoma katika shule hii. Ninaahidi nitahudhuria shuleni kw siku zote za masomo na zile za ziada, endapo kutatokea dharula ya kutohudhuria shuleni nitatoa taarifa kwa uongozi wa shule, nitasoma kwa juhudi zangu zote na kutoa ushirikiano kwa walimu kwa manufaa yangu, wazazi jamii na taifa kwa ujumla, nitazifuata sheria zote za shule na kuzitekeleza kwa mujibu wa shule inavyotaka. Na endapo sitafuata yote yaliyoainishwa hapo juu hatua kali zichukuliwe dhidi yangu.

**Jina ………………………………………………Saini…………………………….Tarehe……………………………………….**

B) Mzazi/Mlezi

Nimesoma sheria, taratibu na kanuni za shule na kuzielewa. Pia ninafahamu jukumu la mzazi/ mlezi la kumsomesha, kumlinda, kumpatia mwanafunzi wangu mahitaji muhimu ya shule na kufuatilia maendeleo ya kijana wangu shuleni na nyumbani kwa kushirikiana na walimu wa shule hii.

Hivyo nmekaa na mtoto wangu na tumekubaliana kufuata na kuzingatia yote yaliyoainishwa hapo juu .Mimi kama mzazi/mlezi nimekubali kwa dhati kusimamia hayo na tutazingatia sheria,kanuni na taratibu zote.

Kijana wangu hana simu ya mkononi na sitampa simu kwa matumizi yoyote,Niko tayari kuwasiliana na kijana wangu pale awapo shuleni kupitia simu ya shule(0715117719)au mwalimu toka shule husika.

**Jina……………………………………………………………………… Saini…………………………………………….**

**Simu namba……………………………………………….. Tarehe…………………………………………….**

Tafadhali soma maagizo/maelekezo na kuyatekeleza kikamilifu.

Medical examination form

Form No. 3

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

PRESIDENT OFFICE
REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT

TUNDURU DISTRICT COUNCIL

RUVUMA REGION
PHONE No. +255(0) 753412885

Mataka Secondary School
P.O.Box 175
**TUNDURU**

Ref.No. MDSS/UKV/99/VOL 1/2021

Date ...........

**To Medical Officer**
.......................................
.......................................
.......................................

REF: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

Please. Examine ............................................. as to his fitness for pursuing Secondary School studies in this school.

General condition of his health:

Eye/Vision ...........................................
Ears/ Hearing.........................................
Mouth/ Speech .......................................
Nose ....................................................
Blood group ..........................................
Stool ....................................................
Urine ....................................................
HB % ...................................................
Leucocytes ...........................................
E.S.R ...................................................
Others ..................................................

MEDICAL CERTIFICATE
I have examined the above named student, consider and recommend him fit/not fit for studies. Special medical recommendation (if any)
.........................................................................................................................
.........................................................................................................................
.............................................................................................

Date ............................

Signature ..........................
Designation ......................

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)
HALMASHAURI YA WILAYA TUNDURU

SHULE YA SEKONDARI MATAKA

MKOA WA RUVUMA
Simu Na. 0715117719

S.L.P 175 TUNDURU
E – mail: matakasecondary@gmail.com

### SHERIA, KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya Mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya Mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayoletwa na Wizara ya Elimu Sayansi na Tekinolojia na Ufundi yenye dhamana ya Elimu nchini na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa Elimu nchini.

Uwapo shuleni Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo:

a) Heshima kwa viongozi, wazazi,wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Mahudurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya joini (Preparation) hata ukiwa nyumbani.
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uwanafunzi wako katika shule hii.
f) Kutunza usafi wa mwili wako, mavazi yako na mazingira ya shule.
g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
h) Kzingatia ratiba ya shule wakati wote.
i) Kutunza mali ya Umma.

Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa Shule:

a) Wizi
b) Uasherati na Ushoga
c) Ubakaji
d) Ulevi na Matumizi ya Madawa ya Kulevya kama vile Bangi, Cocaine, Mirungi, Kubeli n.k
e) Kupigana au Kupiga.
f) Kuharibu kwa Makusudi Mali ya Umma.
g) Kudharau Bendera ya Taifa
h) Kuwa Mjamzito/ Kupata Mimba
i) Kuoa au Kuolewa
j) Kutoa Mimba
k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
l) Kukataa Adhabu kwa Makusudi.
m) Kuwa na simu ya Mkononi.